# “Onjeni Mwone” Visa vya Tumaini na Imani

Hakimiliki 2007
Kutoka na kuwafikia kwa Injili

# “ONJA UONE” VISA VYA TUMAINI NA IMANI

Kitabu cha Mafunzo

Hatimiliki © 2017 Kutoka na Kuwafikia kwa Injili. Haki zote zimehifadhiwa.

Toleo la 2019

**KAMATI YA UANDISHI**

Pat Gustin, Mwenyekiti
Jon Dybdahl
Beverly Thompson
Kip Ault

**MCHAPISHAJI**

Gospel Outreach
P.O. Box 8
College Place, WA 99324
United States
(505) 525-2951
office@goaim.org

**MTAFSIRI**

Moseti Chacha
Simu: +255 712282224
Baruapepe: moseti.chacha@gmail.com

## Kutoka katika Maneno ya Uvuvio

### Msingi wa Wokovu

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12

"[9] Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. [10] Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu." Warumi 10:9, 10

### Msingi wa Dini zisizo za Kikristo

"Kanuni kwamba mwanadamu anaweza kujiokoa mwenyewe kwa matendo yake imejengeka katika msingi wa kila dini ya upagani… Shetani alishapanda kanuni hii. Chochote kinachoshikiliwa, hakiweki kizuizi chochote dhidi ya dhambi" *Desire of Ages,* Uk. 35, 36

## Onja Uone

"Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema; Heri mtu yule anayemtumaini." Zaburi 34:8 Uzoefu unatokana na elimu iliyopatikana kutoka kwenye majaribio. Dini ya majaribio ndiyo inayohitajika wakati huu. "Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema…" Baadhi yao, idadi ni kubwa, wana elimu ya nadharia kuhusu ukweli wa dini, lakini hawajawahi kupata hisia za nguvu ya neema ya kimbingu ibadilishayo katika mioyo yao. Watu hawa ni wazito sana kusikia na kuitikia shuhuda za maonyo, makaripio na maelekezo… Hawajawahi kuonja na kujifunza kwa uzoefu kwamba Bwana yu mwema." 5T pp. 221, 222

Kuna ushuhuda ambao ni dhahiri kwa wote – wale ambao wameelimika sana, na wale ambao hawana elimu kabisa – udhihirisho wa uzoefu. Mungu anatuita kuthibitisha sisi wenyewe uhalisia wa Neno lake, yaani ukweli wa ahadi zake. Anatuita 'tuonje na kuona kwamba yu mwema….' Zaburi 34d:8 Badala ya kutegemea maneno ya mwengine, tunatakiwa kuonja na kuona sisi wenyewe. Anasema kuwa, "Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." Yohana 16:24 Ahadi zake zitatimizwa. Hawatakuwa wameshindwa, wala hawawezi kushindwa kabisa. Na kadiri tunavyomsogelea Yesu, na kushangilia katika ukamilivu wa upendo wake, mashaka yetu pamoja na utusitusi vitaondoka katika nuru ya uwepo wake." Jipatie Amani Moyoni, uk. 111, 112 (kiingereza)

# Yaliyomo

Utangulizi ……………………………………………………………...………………….. 4

Sehemu ya 1: Kuuona Upendo wa Mungu …………………………………………….. 6

Sehemu ya 2: Kupitia uzoefu wa Uweza wa Mungu ……………………………………… 10

Sehemu ya 3: Kukaa karibu na Mungu Kila siku. …………………………………….. 15

Sehemu ya 4: Kuwa muumini ………………………………………………..………… 20

Sehemu ya 6: Kujitayarisha kwa ajili ya Ubatizo ……………………………..…………. 26

Kiambatishi A: Njia mbali mbali za kutumia visa ………………………………………… 36

Kiambatishi B: Kupanua orodha ya visa vya Agano la Kale …………………………….. 38

Kiambatishi C: Visa vya ziada kwa mpanglio wa mada …………………………………. 42

Kiambatishi D: Visa kwa ajili ya Waislamu ………………………………………………… 54

Kiambatishi E: Mada za ziada kwa ajili ya kulea na kufundisha ………………………… 58

Kiambatishi F: Vipingamizi na madaraja ya kitamaduni na kidini ……………………… 60

# UTANGULIZI

Kiini cha kozi hii ni kufanya wanafunzi kati ya wale ambao siyo Wakristo, hasa katika lile dirisha la 10 kwa 40. Imekusudiwa iwe rahisi kujifunza, rahisi kutumia, na rahisi kuhamishia kwa mwingine yeyote, kupitia katika taaluma ya kawaida au kwa maneno ya mdomo au kwa vielelezo wale wanaoona tu.

## “Onjeni Mwone”

Kiini cha masomo haya kwa Ujumla ni “kuonja na kuona’ kwamba Mungu yu mwema. Huu uzoefu binafsi wa upendo wa Mungu na neema yake vinaongoza watu kuwa wanafunzi wa Yesu walio hai maisha yao yote. Ni msingi ambao Imani zote zinajengwa juu yake.

Kuna mtiririko wa masomo ya Biblia ambayo yanafanya kazi vyema kwa watu wenye usuli wa Kikristo. Mwelekeo ni katika:

- Kuwatambulisha kwa Yesu wasio Wakristo – walio na elimu na wasio na elimu
- Kudhihirisha upendo na uweza wa Mungu kupitia katika kuingiliana na kwatumikia kama Yesu alivyofanya, hasa wale waliokandamizwa na kuonewa.
- Kutumia kwa uangalifu visa vya Biblia vilivyochaguliwa kama msingi wa kufundishia kujenga msingi wa Imani na mtazamo wa kidunia wa Biblia.
- Kuwaongoza watu kumwamini Roho Mtakatifu kwa ajili ya uelewa wa Neno la Mungu kisha kufuata kile kilichodhihirishwa.
- Kutia moyo na kuwezesha watu kushiriki na wengine moja kwa moja uzoefu wanaopitia na kile wanachojifunza.
- Kuwaelekeza watu katika nguvu ya maombi na ahadi zilizoko katika Biblia na kuwaongoza kupitia uzoefu wa uponyaji kutoka katika maisha yao yaliyovunjika, pamoja na kuwaweka huru kutoka katika roho wachafu na uraibu.
- Kusaidia watu kutambua na kushughulikia aibu na hatia katika maisha yao, na kupata uhakika wa msamaha na heshima kupitia kwa Yesu.
- Kutambulisha watu kwa Mungu waBiblia kupitia katika kujifunza visa vyake katika Agano la Kale na Agano Jipya.
- Kuwaongoza watu kupata uzoefu wa Mungu kila siku kadiri wanavyojenga maisha ya maombi ya kila siku.
- Kuwaongoza watu katika maamuzi binafsi na kujitoa kikamilifu ili kuwa wanafunzi wa Yesu
- Kuwaleta watu katika makundi ya kujumuika yaliyojikita nyumbani

- Kuwaongoza watu kujitoa kikamilifu, kuwa Wakristo hai waliobatizwa katika kanisa la Waadventista wa Sabato.

Masomo yamejengeka katika **"Hatua za Uanafunzi za Onja Uone"** zifuatazo:

- "Onja Uone" wema wa Mungu kwa kutuchunguza kadiri tunavyochangamana nao
- "Onja Uone" (uzoefu) uwezo wa Mungu katika maisha yao wenyewe kupitia katika maombi
- "Onja Uone" furaha ya kushiriki na wengine ushuhuda binafsi
- "Onja Umwone" (ufahamu) Mungu kwa kusikia visa vya Biblia (Visa vya Mungu) ukiongozwa na Roho Mtakatifu
- "Onja Uone" uwepo wa Mungu kila siku kupitia katika baadi ya uzoefu wa kawaida wa kiroho
- "Onja Uone" uhakika wa furaha ya wokovu kwa kuchagua kuwa mwanafunzi na mfuasi wa Yesu
- "Onja Uone" furaha ya kujumuika na wanafunzi wengine kwa kujifunza mafundisho maalum ya kanisa la Waadventista wa Sabato na kupokea ubatizo.
- "Onja Uone" maisha ya kukua kiroho kwa kuendelea kukua na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi wa Yesu.

**Angalizo kwa Waalimu:** Hatua hizi za Uanafunzi" (tazama hapo chini) ziko ndani ya sehemu sita za kitabu cha mafundisho. Mambo yaliyomo katika **Sehemu ya 1** ni ya msingi kwa mengine yote yanayofuta, hivyo sehemu muhimu ya kuanzia kwa kozi. **Sehemu ya 2 - 5,** inaweza kuwasilishwa kwa mpangilio. Uongozwe na Roho Mtakatifu kuamua ni sehemu gani inateka shauku ya kila mmoja ambaye unajifunza naye. Sehemu ya 1 hadi ya 5 inahitaji kukamilishwa kwanza kwa kuwa ni ya msingi kwa ajili ya somo ka 6 – Kujitayarisha kwa ajili ya Ubatizo

## SEHEMU YA 1:

# KUUONA UPENDO WA MUNGU

### MATAYARISHO

**UTANGULIZI:**

Kwa namna wakulima wazuri wanavyofahamu, ni muhimu kutayarisha shamba kabla ya kupanda mbegu. Kuondoa mawe, kung'oa magugu na kulima udongo. Yote hayo ni sehemu ya matayarisho. Ni muhimu pia kutayarisha udongo wa mioyo ya watu kabla ya kupanda mbegu za injili. Maombi kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kujichanganya na watu, kujenga daraja la uelewa, kupata "mtu wa Amani," na kushiriki ushuhuda binafsi ni baadhi ya sehemu muhimu za matayarisho.

**Omba, Omba, na Omba.**

- Jiombee mwenyewe – omba ili uwe imara na mwenye uwezo wa kumshuhudia Yesu
- Omba ili Roho Mtakatifu akuongoze kadiri unavyojitayarisha kuingiliana na watu
- Omba Roho Mtakatifu atayarishe watu utakaokutana nao
- Omba ili umpate "watu wa amani" – watu ambao watakuwa wamefunguka kiroho ili kupokea mambo mapya ya kiroho
- Omba kuwa kadiri unavyojichanganya, ukifuata mfano wa Kristo wa ukutane na mahitaji ya watu pale walipo
- Omba kwamba upate njia ya kuwasaidia wale walioonewa na kukandamizwa, ambao wananyanyaswa kwa sababu watu hawawaelewi.
- Omba kadiri unavyojenga uhusiano wa kuaminiana na watu.
- Anza kuombea orodha ya watu maalum watatu hadi watano ambao unawaombea ili upate kujenga uhusiano nao
- Omba kila siku ukiombea watu waliopo katika orodha yako na ongezea kwenye orodha yako kila wiki kadiri navyoendelea kuomba.
- Omba upate fursa maalum za kujenga uhusiano na kushiriki na watu wambao hawamfahamu Yesu.

## Kristo alijichanganya na watu na kushughulikia mahitaji yao

### Mbinu za Kristo Pekee

"Dunia leo inahitaji kile ambacho ilikihitaji miaka 1900 iliyopita – Kufunuliwa kwa Kristo... ni kwa kupitia kwa neema ya Kristo tu ndipo kazi ya kuhuishwa kimwili, kiakili, na kiroho inaweza kukamilishwa.

"Mbinu za Kristo pekee ndizo zinazoweza kukupatia mafanikio katika kuwafikia watu. Mwokozi alijichanganya na watu kama mmoja aliyewatakia mema. Aliwahurumia, akashughulikia mahitaji yao, ndipo akateka mioyo yao. Hapo aliweza kuwaambia "Nifuateni."

Kuna haja ya kuja karibu na watu kwa jitihada binafsi. Ikiwa muda unaotumiwa kwa mahubiri ungepunguzwa na muda mwingi ukatumika kwa huduma binafsi, kungekuwa na matokeo makubwa. Masikini wanatakiwa kupewa nafuu, wagonjwa kuhudumiwa, wenye huzuni na waliofiwa kufarijiwa, wajinga kuelekezwa katika uelewa, wasio na uzoefu kushauriwa. Tunatakiwa kulia na wanaolia, na kufurahi na wanaofurahi. Ukiwa na uwezo wa kushawishi, uwezo wa maombi, uwezo wa upendo wa Mungu, kazi hii haitakosa matunda."

*Huduma ya Uponyaji,* uk. 143, 144

**Jichanganye, Jichanganye, Jichanganye**

Kabla watu hawajasikia kuhusu upendo wa Mungu, mara nyingi wanahitaji kuuona upendo huo katika vitendo. Yeyote anayekuwa mwanzilishi wa kazi katika maeneo mapya ambayo hayajafikiwa, ni lazima awe na uzoefu na watu na kujenga uhusiano wenye kuaminiana kupitia katika maombi, kujichanganya, na kutumika kama Yesu alivyofanya. Lengo la kujichanganya siku zote ni ili watu "waonje na kumwona" Mungu kupitia katika huduma yako.

Hapa pana mapendekezo machache ya namna ya kujichanganya na kuhudumu. Utagundua njia zingine zilizo muafaka na maeneo ambapo unafanya kazi, watu unaofanya kazi nao na stadi zako mwenyewe na uwezo wako.

- Wafahamu watu – shauku zao, mahitaji yao, mambo yanayohusu familia, furaha na huzuni, n.k.
- Hudhuria shughuli za familia – sherehe za harusi, mazishi, sherehe za kuzaliwa kwa watoto na siku za kuzaliwa.
- Omba na watu – wagonjwa, waliokata tamaa, wapweke, waliokandamizwa, waliofiwa, n.k.
- Wapatie tiba ya afya iliyo rahisi – kuchua, kuufanyisha mazoezi mwili wako, n.k.

- Jishughulishe na watu katika kazi zao – kulima, kupanda, kuvuna, kusafirisha bidhaa, kuchota maji, n.k.
- Watembelee wagonjwa, na wazee ukiwatia moyo na kuwaelekeza tiba ya afya zao iliyo rahisi.
- Uwe wakili wa wale walioonewa, ambao wananyanyaswa na wale wasioeleweka.
- Jihusishe katika kusaidia kupanga matukio ya jumuiya – maonesho, gwaride, sherehe za sikukuu mbali mbali, n.k.
- Jiunganishe na watoto (wachukue mkatembee baada ya shule, ukiwafundisha katika michezo, visa na hadithi, n.k.)
- Endesha madarasa kwa jumuia (madarasa ya kiingereza, masuala ya fedha, malezi, afya ya msingi, mapishi, n.k.)
- Jiunge na mashirika binafsi yaliyopo sehemu mahalia yanayotoa huduma (kwa mfano msalaba mwekundu, n.k.)
- Ingia katika ubia na wale ambao tayari wanahudumia jamii.
- Fanya kazi katika magereza (watembelee, wapelekee vitu vidogo vidogo vilivyo muhimu, sherehekea siku zao maalum, wahudumie, n.k.)
- Tayarisha "miguko ya upendo" kwa watu wenye mahitaji maalum (yatima, wazazi wasiokuwa na wenzi, wahanga wa ubakaji, n.k.)
- Saidia watu kujifungua hasa kama ni mkunga na kama umeombwa, ukiona kwamba inastahili.
- Panga na kusaidia katika bustani za jumuia.
- Panga shughuli za afya kama vile maonesho ya afya, madarasa ya mapishi, malezi ya watoto, n.k.)
- Panga matamasha ya muziki au Sanaa.
- Panga kambi fupi la vijana (kwa mfano Amani, Sanaa, michezo, au kambi la muziki)
- Wasaidie watu au jumuia kuanzisha shughuli ndogo ya kuweza kuboresha maisha yao
- Omba Mungu afungue macho yako uone fursa mpya.

Kumbuka kwamba lengo ni kumdhihirisha Mungu – kudhihirisha upendo wake, huruma yake, na utukufu wake, lakini huu ni mwanzo tu. Kadiri unavyoenelea kuona uwezekano zaidi pamoja, utagundua njia zingine za kuingiliana na jumuia yako ili kuleta tofauti kwa kufuata sampuli ya Yesu.

**KUJENGA MADARAJA YA UELEWA**

Kadiri tunavyofanya kazi na watu mbali mbali wenye usuli uliotofautiana, na tamaduni tofauti, ni lazima kuelewa mfumo wa Imani yao na baadhi ya vikwazo kati ya utamaduni wao au dini yao na ya kwetu ni lazima tujifunze jinsi ya "kujenga madaraja" kati ya Imani yao na ile ya kwetu. Ni dhahiri kwamba hili ni jambo maalum kwa kila dini na kila utamaduni, kwa hiyo vinatakiwa kushughulikiwa kila kimoja tofauti na kingine. Taarifa bora kabisa kwa kila dini iliyoko duniani zinaweza kupatikana katika tovuti hii hapa chini: [www.globalmissioncenters.org](http://www.globalmissioncenters.org) Ziada ya vyanzo ni kitabu kilichoandikwa na Paul Dybdahl, "Before We Call Them Strangers: What Adventist Out to know about Muslim, Buddhists, and Hindus. Pia kuna angalizo la kuchukulia maanani katika kiambatishi D kwa ajili yako kutumia unapoanza kukusanya taarifa zenye thamani.

**KUTAFUTA "WATU WA AMANI"**

Katika kila jumuiya Mungu anatayarisha watu wa kumpokea. Watu hawa wako wazi kiroho na tayari kupokea uongozi wa Mungu. Omba kwamba Roho Mtakatifu akuongoze kwa watu hawa. Wanaweza kuwa niwatu wanaoitikia kwa namna iliyo chanya kwa kuomba pamoja. Wanaweza kuuliza maswali au kuanzisha mazungumzo (wala siyo mabishano) au wakati mwingine kuonesha shauku katika mambo ya kiroho au mada za kidini. Maeneo mengine, watu wameshakuwa na maono au njozi au hata uzoefu wa pekee ambao umewatayarisha kuitikia kwa namna iliyo chanya. Kadiri tunavyojichanganya na watu, tunaomba kwamba Roho Mtakatifu atuongoze kwa "watu wa amani" ambao Mungu amewatayarisha. Hawa watiakuwa na uwezekano mkubwa wa kupokea kadiri tunavyoshiriki shuhuda zetu.

**JITAYARISHE KUSHIRIKI USHUHUDA WAKO MWENYEWE**

Kumbuka kisa cha yule aliyepagawa na mapepl katika Marko 5:18-20? Hakujua chochote kuhusu mafundisho au Imani, lakini Yesu alimtuma kushuhudia kwa watu wa nyumbani kwake, akimwambia kuwa, "… Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu." Je, Mungu amekutendea mambo gani? Je Yesu aliye hai ameleta tofauti gani katika maisha yako? Kadiri unavyoendelea kuwafahamu watu, na kukuza uhusiano nao, moja ya mambo yenye nguvu unayoweza kushiriki ni ushuhuda wako binafsi au uzoefu wako. Ni lazima ujielekeze kwa Yesu – upendo wake, rehema zake, na nguvu zake katika maisha yako. (tazama sehemu ya 2 kwa mapendekezo ya jinsi unavyoweza kutayarisha ushuhuda wako binafsi na kushiriki na wengine.

**SEHEMU YA 2:**

# KUPITIA UZOEFU WA UWEZA WA MUNGU

**"Onjeni Mwone"**

**UTANGULIZI:**

Ili watu wajenge Imani iliyo thabiti kwa Mungu, ni lazima wawe na uzoefu binafsi na nguvu za Mungu katika maisha yao. Manabii katika Maandiko walitazamia kwamba Mungu ataonesha nguvu zake "ili kwamba mataifa (ya waisoamini) yatambue kwamba wewe ni Mungu." (Ezekieli 36:22-24) Visa vilivyopo katika sehemu ya pili vinatupatia fursa ya kushiriki katika uzoefu wa watu wengi walio katika Biblia ambao walipitia uzoefu binafsi wa Uwezo wa Mungu katika maisha yao. Yesu alidhihirisha uwezo wa Mungu anayependa katika miujiza mingi aliyotenda ya uponyaji na ukombozi. Imani ya msingi ya waumini wa mwanzo ilikuwa katika nguvu ya kufufuka kwa Kristo (Warumi 10:9, 10). Somo lililopo katika sehemu hii linadhihirisha namna nyingi ambazo watu wanapitia uzoefu wa nguvu za Mungu, kuanzia kwako WEWE – namna ambavyo umepitia uzoefu wa Kristo katika maisha yako.

**Fundisho la 1: Shiriki ushuhuda au uzoefu wako mwenyewe.**

Je, Yesu aliye hai ameleta mabadiliko gani katika maisha yako binafsi? Ushuhuda wako ni lazima ujielekeze kwa Yesu – siyo kwako mwenyewe au kwa mtu mwingine, au hata kwa kanisa au katika ukweli uliojifunza kanisani kwako. Ni lazima ujielekeze kwa Yesu na upendo wake na uwezo wake katika maisha yako. Ikiwa ulizaliwa katika familia ambayo haikuwa ya Kikristo au tangu ulipokuwa Mkristo, ni magumu gani au changamoto gani ambazo Kristo ameshakusaidia? Je, ni maombi gani ambayo Mungu ameshajibu?

Ushuhuda wako unatakiwa kuwa mfupi – kama dakika tatu hivi – na unahitaji kueleza kwa shauku na kwa namna iliyo dhahiri. Andika kwenye karatasi, au weka muhutasari kabla haujaelezea. Ikiwezekana fanyia mazoezi ukishirikiana na mtu mwingine ambaye anaweza kukusaidia kuelezea vyema zaidi.

Utakuwa na uzoefu zaidi ukionesha uwezo wa Yesu. Siku zote chagua ushuhuda ambao unaendana na mtu yule anayesikiliza.

**Angalizo kwa Mwalimu: Visa vya watu waliopitia uzoefu wa nguvu za Mungu katika maisha yao**

Masomo ya 2-12 katika sehemu hii, yamejengka katika visa vya Biblia vya "Onjeni Muone" vinavyoonesha jinsi nguvu za Yesu zilivyoleta tofauti katika maisha ya watu waliomwamini (waliomjaribu)

Visa hivi vilichaguliwa ili kuonesha nguvu za Mungu katika maeneo mbali mbali ya maisha. Kuna visa vingi katika Biblia vya jinsi ambavyo Yesu aliponya watu. Watu wengi katika dunia yetu leo wamevunjika katika maisha yao na wanataka uponyaji – wa kimwili, kiroho, na kumhemuko. Kuna haja pia ya upinyaji wa mahusiano katika familia, katika ndoa, na katika mataifa kwa ujumla.

Watu wengi wanaishi na aibu, hofu, na hatia. Yesu ni mponyaji wa mambo yote haya. Yeye anatka kutuponya ili kwambatuweze kuishi maisha yenye heshima, furaha, na Amani. Shiriki kisa chako na kuwaongoza watu kuomba wapate uwezo wa Mungu uletao uponyaji katiak maisha yao wenyewe au katika maisha ya mtu mwingine mnayempenda.

**Tumia "Hatua za kujifunza/kushiriki kisa" katika uk. 11.** Baada ya kujifunza kila kisa, jifunze fungu la kukariri pamoja kama namna ya kujikumbusha uwezo wa Mungu

**Fundisho la 2: Muuaji aliyebadilishwa** (Matendo 9:1-11, 17, 18). Sauli alibadilishwa kutoka kwa muuaji na kuwa Paulo ambaye ni mfuasi wa Yesu.

- Fungu la Kukariri: Ezekieli 36:36

**Fundisho la 3: Toka katika uoga hadi kwenye ushujaa** (Matendo 4:17-23, 29-31). Waumini walikuwa waoga kwa sababu ya vitisho vya viongozi, lakini walikuwa jasiri na kuondoa uoga kupitia kw uwezo wa Mungu, na Mungu alifanya miujiza katika kujibu maombi yao.

- Fungu la Kukariri: Zaburi 34:19

**Fundisho la 4: Toka katika kukata tamaa hadi kuwa na matumaini** (Luka 24:13-32). Hawa watu wawili hawa walijawa na uoga, wakiwa wamechanganyikiwa na kukata tamaa, lakini baada ya kukutana na Yesu, mioyo yao ilipata fukuto na wakajawa na ujasiri na tumaini.

- Fungu la Kukariri: Wafilipi 4:6, 7

**Fundisho la 5: Kuponywa kwa mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu** (Marko 5:24-34). Mwanamke huyu alikuwa mgonjwa kwa muda wa miaka 12, lakini alipata uponyaji wa adha yake kupitia kwa uwezo wa Yesu

- Fungu la Kukariri: Yeremia 17:14

**Fundisho la 6: Kuponywa kutoka katika pepo waovu, laana, na dhami za vizazi.** (Luka 4:31-37) Yesu alimponya mtu aliyekuwa amepagawa katika sinagogi

- Fungu la Kukariri: Luka 4:36

**Fundisho la 7: Yesu anaponya magonjwa mbali mbali** (Luka 4:38-41)

- Fungu la Kukariri: Yakobo 5:14

**Fundisho la 8: Yesu anaponya kutoka katika dhambi, aibu na uraibu.** (Yohana 8:1-11) Yesu aliponya na kusamehe mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi.

- Fungu la Kukariri: Isaya 1:18

**Fundisho la 9: Yesu anaponya kutoka katika hofu ya nguvu za asili** (Marko 4:35-41) Amani katika dhoruba

- Fungu la Kukariri: Yohana 14:27

**Fundisho la 10: Yesu anaponya kadiri tunavyopitia katika uzoefu wa upendo wa Mungu** (Luka 15:11-24)

- Fungu la Kukariri: Marko 1:41

**Fundisho la 11: Yesu anaponya kadiri tunavyopokea uzoefu wa msamaha** (Luka 7:36-48). Mwanamke aliyepaka mafuta miguu ya Yesu

- Fungu la Kukariri: Marko 2:5

**Fundisho la 12: Yesu anatuponya kadiri tunavyokuwa na Imani na tumaini** (Marko 10:46-52) Kumponya kipofu Batimayo

- Fungu la Kukariri: Marko 10:52

**Angalizo kwa Mwalimu: Kuwaongoza watu kudai ahadi za Mungu**

Kariri mafungu ya kila sehemu. Endelea kuwatia moyo watu kuwa na tafakuri ya kila siku kuhusu Maandiko kadiri wanavyojifunza. Katika kila somo kadiri Roho Mtakatifu anavyoongoza unaweza kuwahimiza watu "Kumjaribu Mungu" katika maisha yao wenyewe kwa kutumia maswali kama:

- "Je ungependa kuwa na uzoefu binafsi na Mungu aliye hai au Yesu?"
- "Je, uko tayari kumjaribu Yesu uone kama yu hai?"
- "Ungependa usaidiwe nini katika maisha yako? Je, una wasi wasi? Una mfadhaiko? Ni mraibu? Au Unaumwa?"
- "Je, unataka Amani? Furaha? Upendo? Unahitaji msaada katika mahusiano? Masuala ya Fedha? Kazi? Yesu anaweza kukusaidia."

Hata kama watu hawataamini mwanzoni, waongoze katika kuanza kuomba uwezo wa Yesu katika maisha yao. Wahimize kuomba asubuhi na usiku kwa wiki mbili na kuona ni nini kitakachotokea. Waoneshe namna ya kutumia ahadi za Mungu zilizopo katika Biblia (hapa chini) kadiri wanavyoomba.

## Ahadi za Mungu kwenye Biblia

**Utangulizi:**

Mara nyingi katika Biblia, Mungu/Yesu aliwaahidi watu wake mibaraka. Wakati mwingine hawa watu "hawakuona" mibaraka au ahadi moja kwa moja. Walitakiwa kuamini hizo ahadi na kuzikubali, kisha wakapokea mibaraka.

Kisa kizuri kinachoonesha hili ni Luka 17:11-19. Soma na kujafili kisa hiki kwa kutumia DBS. Kisha uliza kuwa, "Walitaka nini?" "Yesu naye alisema nini au alifanya nini?" "Ni wakati gani walipoponyw? Waliitikia na kutenda wakijenga katika ahadi kwanza kabla hawajaponywa, kisha wakapokea mibaraka. Ndivyo tunavyodai ahadi za Mungu.

Hapa chini kuna baadhi ya ahadi ambazo Yesu aliwapa wafuasi wake. Chagua moja ya hizi ahadi na uzitumie katika maombi.

- **Kwa Amani:** Yohana 14:27 "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga."
- **Kwa furaha:** Yohana 15:11 "Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe."
- **Kwa tumaini:** Zaburi 42:11 "Nafsi yangu, kwa nini kuinama, Na kufadhaika ndani yangu? Umtumaini Mungu; Kwa maana nitakuja kumsifu, Aliye afya ya uso wangu, Na Mungu wangu."

- **Kwa msaada wakati wa shida:** Zaburi 34:19 "Mateso ya mwenye haki ni mengi, Lakini Bwana humponya nayo yote."
- **Kwa ulinzi:** Mithali 18:10 "Jina la Bwana ni ngome imara; Mwenye haki huikimbilia, akawa salama."
- **Kwa wasiwasi:** Wafilipi 4:6, 7 "[6] Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. [7] Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."
- **Kwa uoga:** Isaya 41:13 "Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia."
- **Kwa hofu ya kifo:** Zaburi 23:4 "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji."
- **Kwa upweke:** Yohana 14:18 "Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu."
- **Kwa hisia za aibu:** Warumi 10:11 "Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika."
- **Kwa kujaribiwa kutenda uovu:** Warumi 6:14 "Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema."

**SEHEMU YA 3:**

# KUMFAHAMU MUNGU NA KUPATA UZOEFU WAKE KUPITIA KATIKA KISA CHAKE

## UTANGULIZI:

Namana iliyo bora ya kuwafhamu watu ni kwa kusikia visa vyao. Maisha yetu ni mkusanyiko wa visa vyetu sisi wenyewe. Kadiri tunavyojitambulisha watu kutoka katika chimbuko lisilo la Kikristo kwa Mungu wa Biblia ni lazima kwamba wamfahamu kabla hatujawaambia wamtii. Tabia yake, utambulisho wake vinadhihirishwa katika mamia ya visa vilivyoorodheshwa katika Biblia. Visa vya Agano la Kale vinaonesha jinsi alivyoingiliana na watu mmoja mmoja na pia taifa la Israeli katika mazingira yaliyokuwa chanya na hata yaliyokuwa hasi. Visa vya Agano Jipya vinajielekeza katika maisha ya Yesu, aliye Mwana wa Mungu, ambaye alikuja kumfunua Mungu kwa walimwengu. Lengo la kujifunza visa hivi ni kuwatambulisha watu kwa Mungu – kile ambacho kila kisa kinadhirihirisha kumhusu. Hata kwa Wakristo wenyewe, kuangalia visa hivi kwa namna iliyo mpya kutakuwa na manufaa kwao.

**Angalizo kwa Waalimu:**

Visa hivi viko kwa mpangilio – ukianza na kisa cha uumbaji katika kitabu cha Mwanzo na kumalizia na kisa cha dunia mpya kitabu cha Ufunuo. Visa hivi vinakupatia mtazamo wa haraka wa jinsi Mungu anavyoshughulika na watu akidhihirisha tabia yake ya upendo.

Baadhi ya watu wanaweza kuvutiwa na kisa cha Yesu, na hapo basi pengine utachagua kuanza na visa vya Agano Jipya katika Biblia kabla haujaingia katika visa vya Biblia katika Agano la Kale. Jambo la muhimu ni kutumia visa vyote (vya Agano la Kale na Jipya) kadiri unavyowatambulisha watu kwa Mungu wa Biblia.

Majina au visa vilivyooneshwa kwa maandishi mazito vimetajwa kwenye Quran pia.

Lengo ni kufanya yafuatayo:

- Kufahamu na kupitia uzoefu ("Onjeni mwone") wa Mungu kupitia katika kujifunza kisa chake.
- Kuanza kujenga mtazamo wa kidunia wa Biblia na msingi wa elimu ya Biblia kama msingi wa Imani na tumaini.
- Kujifunza kumsikiliza Roho Mtakatifu kadiri anavyotufundisha.
- Kujifunz akumtumaini Mungu wa Biblia na kisha kutii kile tunachojifunza.

**Hatua za kujifunza/kushiriki kisa**

1. Omba ili upate uongozi wa Roho Mtakatifu
2. Soma kisa pamoja (au elezea hicho kisa)
3. Pitia pamoja katika kikundi ili kukumbuka mambo kwa undani.
4. Rudia kusoma na kuelezea tena; waambie watu wafunge macho yao na "kuona" hicho kisa. Kisha kila mmoja ashiriki kile anachosema kwamba "ameona."
5. Uliza maswali na kufanya kikundi kujadili pamoja. Kila mmoja anaweza kushirikishwa katika mjadala.
    - Uliza: "Je, kisa hiki kinatuonesha/kinatufundisha nini kuhusu Mungu?
    - Uliza: "Je, kisa hiki kinatuonesha/kinatufundisha nini kuhusu wanadamu? Kutuhusu sisi wenyewe? Kuhusu chaguzi ambazo watu wanafanya?
    - Uliza: "Je, ninajifunza nini kutoka katika kisa hiki ambacho ninatakiwa kufuata au kutii?
    - Uliza: "Je, ni nani ninayeweza kushiriki naye kisa hiki

**Visa vya Agano la Kale**

Somo la 1: **Uumbaji**
    Mwanzo 1:1–2:3 (Kisa kwa muhutasari)
Somo la 2: Kuanguka kwa **Adamu** na **Hawa**
    Mwanzo 3:1–15
Somo la 3: **Kaini** na **Habili** – Dhambi na aibu vinaijaza dunia
    Mwanzo 4:1-12
Somo la 4: Mungu anamuonya **Nuhu**
    Mwanzo 6:5-11
Somo la 5: **Nuhu** anamtii Mungu
    Mwanzo 7:5-22
Somo la 6: Mungu anaweka agano na **Nuhu**
    Mwanzo 8:20-22; 9:12-17
Somo la 7: **Mnara** wa Babeli
    Mwanzo 11:1-9
Somo la 8: Mungu anazungumza na **Abraham**
    Mwanzo 12:1-7
Somo la 9: **Sara** na **Abrahamu** wanahidiwa mtoto
    Mwanzo 18:1-15
Somo la 10: **Abrahamu** na **Isaka** na kondoo wa kafara.
    Mwanzo 22:1-18

Somo la 11: Familia ya **Isaka**

Mwanzo 24:36 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 12: **Yakobo** na **Yusufu** na kaka zake.

Mwanzo 37:1-11

Somo la 13: **Ayubu**

Ayubu 1, 2 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 14: Kuzaliwa kwa **Musa** na maisha yake ya mwanzo

Kutoka 2:1-15 (Kutoka moja ni maelezo kwa usuli)

Somo la 15: Mungu anamwita **Musa** (kichaka kinachowaka moto)

Kutoka 3:1-12

Somo la 16: Mapigo tisa ya mwanzo

Kutoka 7-10 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 17: Pasaka inaanzishwa

Kutoka 12-21-30

Somo la 18: Kuvuka bahari ya Shamu

Kutoka 14:21-31 (Kutoka 14:5-14 ni ni maelezo kwa usuli)

Somo la 19: Mungu anawapatia maji na chakula

Kutoka 17:1-7 (Kutoka 16 ni maelezo kwa usuli)

Somo la 20: Mungu anawapatia sheria katika mlima Sinai

Kutoka 20:1-17

Somo la 21: Kujenga Hema ya kukutania

Kutoka 25-27 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 22: Siku ya Upatanisho

Walawi 16:29-34 (Walawi 16:1-28 ni maelezo kwa usuli

Somo la 23: Gidioni na mashujaa 300

Waamuzi 6-8 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 24: **Daudi** na **Goliath**

1 Samweli 17

Somo la 25: **Daudi** na uzao wake

1 Samweli 7:8-17; Isaya 9:6-7

Somo la 26: Hekima ya Sulemani

1 Wafalme 3:7-9, 16-27 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 27: **Yona**

Yona 1-4 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 28: **Danieli** na rafiki zake wakiwa utumwani

Danieli 1:1-20

Somo la 29: Danieli anamtii Mungu

Danieli 6 (kisa kwa muhutasari)
Somo la 30: Malkia Esta ni mwaminifu
Esta 2:1-18, 3, 4, 7-9 (kisa kwa muhutasari)

**Visa vya Agano Jipya**

Somo la 1: Unabii wa Mtumishi anayeteseka
Isaya 53:1-10
Somo la 2: Malaika wamtokea **Mariamu**
Luka 1:26-30
Somo la 3: Kuzaliwa kwa **Yesu**
Luka 2:1-14
Somo la 4: Ugeni wa Mamajusi
Mathayo 2:1-12
Somo la 5: **Yohana** atangaza Njia iliyonyooka
Yohana 1:19-28
Somo la 6: Ubatizo wa **Yesu**
Yohana 1:29-35
Somo la 7: **Yesu** amponya mtu aliyepooza
Marko 2:1-12
Somo la 8: **Yesu** akutana na **Nikodemu**
Yohana 3:1-8
Somo la 9: **Yesu** na **Sabato**
Marko 2:23-3:6
Somo la 10: Yesu amponya kiwete, kipofu, wakoma na bubu
Mathayo 15:29-31
Somo la 11: Yesu na rafiki zake, Mariamu, Martha, na Lazaro
Luka 10:38-42
Somo la 12: Yesu afundisha kuhusu ufalme wa Mungu
Mathayo 13:31-34, 44-52
Somo la 13: Kifo na ufufuo wa Lazaro
Yohana 11-1-43 (kisa kwa muhutasari)
Somo la 14: Yesu ndiye Njia, Kweli na Uzima
Yohana 14:1-11
Somo la 15: Chakula cha mwisho
Yohana 22:7-22
Somo la 16: Yesu katika bustani ya Gethsemani

Mathayo 26:36-46

Somo la 17: Yesu atiwa mikononi mwa watesi na kushitakiwa

Luka 22:47-23:11 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 18: Kifo cha Yesu

Yohana 19:16-35 (kisa kwa muhutasari)

Somo la 19: Kufufuka kwa Yesu

Luka 24:1-9

Somo la 20: Yesu yu hai na anawatokea wanafunzi wake

Mathayo 28:1-20

Somo la 21: Maneno ya mwisho ya Yesu

Matendo 1:4-11

Somo la 22: Mtu kiwete aponywa na Petro na Yohana

Matendo 3:1-10

Somo la 23: Kuongolewa kwa Paulo

Matendo 9:1-19

Somo la 24: Paulo avunjikiwa na meli

Matendo 27:13-44

Somo la 25: Mbingu mpya na Nchi mpya

Ufunuo 21:1-8

**SEHEMU YA 4:**

# KUPITIA UZOEFU WA YESU SIKU KWA SIKU

## UTANGULIZI:

Kila siku katika maisha yetu yote, ni muhimu kuendelea kupitia uzoefu wa uwezo wa Yesu wa kutuponya na kutubadilisha. Kuna mambo sita ambayo tunaweza kufanya kila siku yanayoweza kutusaidia kubaki tumeunganika na Yesu na uwezo wake. *Haya mambo siyo miujiza au kaida fulani ambazo tunatakiwa kufanya ili kumridhisha Mungu*. La hasha! Kama vile tunavyokula chakula, tunavyokunya maji masafi, tunavyopumua hewa safi na kufanya mazoezi ili kukua, na kuwa wenye afaya na imara kimwili, ndivyo ilivyo pia tunapofuata kanuni za msingi za utendaji ili kukua na kuimarika kiroho.

> **Angalizo kwa Waalimu:**
>
> Pamoja kisa kwa kila somo, kuna fungu la kukariri kama sehemu ya tafakuri yetu kila siku. Mwisho wa kila somo, waombe wafanye maamuzi/kujitoa kikamilifu kufuata utendaji huu kila siku. Pitia na kuhimiza uwajibikaji kila wiki. Endelea kutumia hatua hizi kwa ajili ya kushiriki kisa kilichopo uk. Wa 9

**Somo la 1: Toba na Maungamo:** Kadiri mtu anavyokuwa muumini, ni muhimu kutubu na kuungama dhambi. Dhambi inafanana na sumu. Tiba yake pekee ni Yesu. Ni pale tu tunapokiri aibu yetu na dhambi na kumwomba Yesu aiondoe ndipo tunapoweza kuwa waumini imara. Tunatakiwa kuungama dhambi zetu kila siku kwa Mungu ili tupate kusamehewa.

| | |
|---|---|
| Visa: | Toba: Zakayo katika Luka 19:1-10 |
| | Maungamo: Daudi katika 2 Samweli 12:13, 14 |
| | Msamaha: Mwana mpotevu katika Luka 15:`17-21 |
| Fungu la Kukariri: | Marko 1:15; Yakobo 1:5 |

**Somo la 2: Maombi na Tafakuri:** Omba na kutafakari katika Neno la Mungu mara mbili au tatu kwa siku

| | |
|---|---|
| Visa: | Yesu katika Marko 1:35-37 |
| | Danieli katika Danieli 76:3-10 |
| Fungu la kukariri: | Zaburi 119:15 |

**Somo la 3: Ibada na sifa:** Roho ya shukurani na sifa kwa Mungu ni sehemu ya mchakato wa kukua.

Kisa: Mkoma mwenye shukurani katika Luka 17:11-19

Fungu la kukariri: Zaburi 9:1, 2

**Somo la 4: Kujumuika:** Uwe sehemu ya kundi la kudumu siku ya Sabato na siku zingine zitakazochaguliwa. Ikiwa tunahitaji kuwa imara ni muhimu kujumuika na waumini wengine

Kisa: Kanisa la awali (Matendo 2:41-47)

Fungu la Kukariri: Waebrania 10:24, 25

**Somo la 5: Pendaneni ninyi kwa ninyi.** Kuishi ile amri ya Yesu isemayo kuwa, "Mpende jirani yako kama nafsi yako" (Mathayo 22:35-39). Uwe tayari kujifunza kuwapenda wengine, hata kama ni adui zako. Kufanya hivi kunafungua moyo wako kupokea upendo wa Mungu zaidi na zaidi.

Kisa Msamaria Mwema katika Luka 10:25-37

Fungu la kukariri: Yohana 15:12, 13

**Somo la 6: Kuuishi Utume mkuu**. Shiriki kile uzoefu unaopitia. Kushiriki ni kama kufanya mazoezi: Kunakusaidia kuimarika.

Kisa: Mtu aliyepagawa na mapepo katika Marko 5:1-20

Fungu la kukariri: Mathayo 28:19-20

**SEHEMU YA 5:**

# KUWA MUUMINI

**UTANGULIZI:**

Baada ya watu kuanza kupitia uzoefu wa uwezo wa Yesu katika maisha yao, na kadiri wanavyomfahamu Mungu kupitia katika kisa chake, watakuwa wameiva kuwa waumini. Waumini ni watu waliochagua kumtumaini Yesu na kumfuata. Wanajua kwamba atakuwa pamoja nao siku zote – akiwa jali, akiwaongoza, akiondoa aibu yao, na kuwaooa kutoka katika mauti ya milele. Visa vya Biblia vifuatavyo vinahusu watu ambao waligeuka na kuwa waumini.

**Angalizo kwa Waalimu:**

Kadiri Roho Mtakatifu atakavyokuongoz, shiriki visa vya namna watu walifanya uamuzi kuwa waumini/kumfuata Yesu. Somo la 6 lina namna tatu za kuwafanya watu wafanye uamuzi. Chagua kwa maombi njia ile inaonekana kuwa bora zaidi, au tengeneza ya kwakao mwenyewe. Ni muhimu kwa watu kufanya uamuzi na kisha kuomba ombi la kukubaliwa na kujitoa kikamilifu. Endelea kufuata hatua za kushiriki kisa zilizopo uk. Wa 8

**Somo la 1: Mtu chini ya mlima mrefu:** (Marko 9:14-25). Mtu huyu alitaka kuamini, lakini ilikuwa vigumu. Alihitaji msaada wa Yesu ili awe muumini. Tunaweza kuomba ombi hili sisi pia.

- Fungu la kukariri: Marko 9:24

**Somo la 2: Mlinzi wa gereza kule Filipi:** (Matendo 16:25-34). Mtu huyu alichunguza maisha ya Paulo na kusikia ushuhuda wao. Yeye na familia yake yote waliamini nao wakaokoka.

- Fungu la kukariri: Matendo 16:31

Somo la 3: Tomaso mwenye mashaka: (Yohana 20:24-29). Tomaso hakuamini hadi pale alipoona na kumgusa Yesu. Yesu aliwasifu watu ambao wanaamini hata kabla hawajaona na kumgusa Yesu.

- Fungu la kukariri: Yohana 20:29

**Somo la 4: Mjane wa Serapta**: (1 Wafalme 17:10-16). Mwanamke huyu aliabudu miungu mingine, lakini alikuwa muumini baada ya kuona uwezo wa Mungu katika maisha yake na maisha ya Eliya.

- Fungu la kukariri: 1 Wafalme 17:24

**Somo la 5: Naaman** (2 Wafalme 5:1-10, 14-16). Naaman aliabudu miungu mingine, lakini alichagua kuwa muumini alipopitia uzoeru wa uwezo wa Mungu wa kweli katika kuponywa kwake.

- Fungu la kukariri: 2 Wafalme 5:15

**Somo la 6: Nebukadnezar**: (Danieli 4:4-37 – kisa kwa muhutasari). Nebukadneza alikua mfalme mwenye kiburi na majivuno. Aligeuka akawa muumini pale alipoona kazi za miujiza ya Mungu.

## Ukaribisho ili uwe Muumini

Kadiri Roho Mtakatifu atakavyoongoza, wakaribishe watu wajitoe kuwa waumini na wamkubali Yesu katika maisha yao

“Unaweza kuamua kumwamini Yesu sasa hivi, kama wengine wanavyofanya, na mimi nitakuongaoza katika ombi la kumkubali Yesu. Ikiwa unaona hujawa tayari leo, unaweza kujifunza zaidi na kufanya uamuzi kadiri unavyoelewa zaidi kuhusu kisa cha Yesu.”

- **Wito wa 1 wa kufanya maamuzi:** Uliza kwamba, “Je, kuna wakati unajisikia kukata tamaa kwa sababu kuna dhambi, na aibu katika maisha yako? Ungependa kupata njia ya kutoka katika hali hiyo na kuokolewa kutoka katika aibu ya dhambi?” Unaweza kupitia upya kisa cha “Mwana Mpotevu” katika Luka 15:11-24. Kisha unaweza kusema kuwa, “Unaweza kufanya uamuzi kama yule mwana mpotevu na kumrudia Mungu. Omba ombi hili, na Mungu atakukubali.”

  **Ombi:** “Mimi sistahili kuwa mtoto wako. Ninaamini kwamba umeniokoa kutoka katika dhambi na aibu yake pale ulipokufa na kufufuka kutoka kwa wafu. Sasa ninaamini kwamba utahuisha ndani yangu heshima na hali ya kuwa mtoto wako. Amina.”

- **Wito wa 2 wa kufanya maamuzi:** “Watu wengi wanapatttaaa tttaaaabu kuhisi uhakika wa wokovu. Uliza kwamba, “Je, kuna wakati unahisi kutokuwa na uhakika kwamba Mungu anakuoenda na kwamba atakuokoa? Unakuwa na mashaka kuhusu siku ya hukumu? Hebu nikupe kisa cha jinsi unavyoweza kufahamu kwamba umeokolewa na kukubaliwa na Yesu.” Tumia kisa cha Paulo (kilchojengeka katika 1 Wakorintho 15:1-9 na Warumi 10:9, 10)

Paulo alikuwa mwalimu na kiongozi wa wat wengi ambao walkuwa ni wamini wapya katika Yesu. Walitaka kuwa na maisha mapya yenye heshima. Lakini hawakuwa na uhakika namna ya uokolewa kutoka katika aibu na dhambi. Paulo alitaka kuwasaidia kuishi maisha ambayo yangemheshimu Mungu. Kwa sehemu kubwa Paulo aliwataka wafahamu kwamba Yesu alikuwa anawapenda na alikuwa tayari ameshawaokoa kutoka katika aibu na dhambi."

Paulo alisema kuwa, "Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiri; … Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara; baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote; na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake."

Hii ndiyo habari njema: "… ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Yeyote aaminiye katika yeye, hatatahayari."

**Ombi:** "Ee Yesu, ninaamini moyoni mwangu kawamba ulifufuka kutoka katika wacu. Ninataka kukiri kwa kinyw achangu kwamba wewe ni Bwana! Ninafahamu kwamba sasa nimekubaliwa katika familia yako. Amina."

- **Wito wa 3 wa kufanya maamuzi:** Kisa katika wito huu ni kisa kinachofaa kwa Waislamu. – hiki ni kisa cha kwanza na cha mwisho cha kutoa kafara.

Mungu aliumba ulimwengu ulio mkamilifu kwa ajili ya mtu wa kwanza Adamu na mwanamke wa kwanza, Hawa. Mungu aliwapatia heshima kwa kuwafanya kuwa watawala wa dunia hii. Waliishi katika bustani nzuri ya Edeni. Maisha yao yalikuwa huru kutoka katika uoga, aibu na hatia. Waliishi katika upatanifu mkamilifu na kila mmoja wao pamoja na Mungu, na pia mazingira yaliyokuwa yakiwazunguka. Wakati wote walipodumu kuwa watiifu wa Mungu, wangeendelea kuishi milele.

"Lakini Shetani aliyekuwa ameshaanza uasi kule mbinguni, alikuja na kuwajaribu Adamu na Hawa na kuwafanya wajenge mashaka kumhusu Mungu na hivyo kumtii yeye badala ya Mungu. Adam na Hawa walitenganishwa kutoka kwa Mungu na kupoteza heshima yote waliyokuwa wamepewa. Sasa walikuwa uchi,

na wenye aibu. Kwa hiyo wakatafuta majani ya miti wakafunika uchi wao na aibu yao.

“Mungu angeweza kuwaangamiza mara moja, lakini badala yake aliwapa nafasi ya pili. Aliua mnyama na kuwatengenezea mavazi ya kufunika uchi wao badala ya majani ya miti. Akawapa ahadi ya ajabu, “siku moja mwana wangu atakuja duniani na kuharibu nguvu za Shetani. Atakufa kama kafara kwa ajili yenu na kwa kufa kwake atachukua aibu na dhambi yenu, kisha atawarejeshea heshima na hali ya kukosa hatia.”

Kwa miaka mingi Adamu na Hawa walisubiri ahadi hiyo, wazawa wao walisubiri hiyo ahadi ya ujio wa Mowkozi. Hatimaye alizaliwa na Mariamu na mume wake aliyeitwa Yusufu. Walimpatia jina la Yesu.

“Mambo ya kushangaza yalitokea wakati wa kuzaliwa kwake. Watu wengi waliamini kwamba yule Mwokozi aliyeahidiwa alikuwa amezaliwa, Yesu aliishi duniani kwa zaidi ya miaka 30, akiwasaidia watu na kuwarejeshea afya na heshima.

“Siku moja viongozi walimshika, wakamtesa na hatimaye wakamuua. Alipokufa, wafuasi wake walichanganyikiwa. Ni kwa nini mtu mzuri kama huyu alikufa kifo cha aibu namna hii? Walisahau ahadi kwamba Mwokozi angetolewa kafara kwa dhambi zao.

“Baada ya siku tatu, Yesu alifufuka na kuurudia uhai wake, kisha akapaa mbinguni. Kabla hajaondoka aliwaahidi kwamba angerudi siku moja na kuwachukua kwenda mbinguni. Aliwaambia pia kwamba wanatakiwa kwenda na kuwaambia watu kila mahali kuhusu kafara yake. Ili kukubali hii kafara ya Kristo kwa ajili yako, ninakukaribisha uamini na kumkubali Yesu sasa hivi.

Ombi: “Ee Yesu ninaamini moyoni mwangu kwamba ulikufa kama kafara kwa ajili ya dhambi zangu na ukafufuka kutoka katika wafu. Nataka kukiri na kuungama kwa kinywa change kwamba wewe ni Bwana! Ninaamini kwamba umeniokoa kutoka katika dhambi zangu na aibu yangu, na kwamba utanihuisha na kunirudishia heshima ya kuwa mwana wako. Ninaamini kuwa sasa ninakubalika katika nafasi ya heshima kwenye familia yako. Amina.”

**SEHEMU YA 6:**

# KUJITAYARISHA KWA AJILI YA UBATIZO

## UTANGULIZI:

Katika hatua hii, watu huwa wanapata taabu kumfahamu Mungu wa Biblia.

- Wameona upendo wa Mungu na uwezo wake katika huduma yako
- Wameonja na kupata uzoefu wa uwezo wa Mungu na uponyaji katika maisha yao.
- Wamehimizwa kushiriki na wengine kile walichojifunza na uzoefu waliopitia
- Wamekuwa wakijenga msingi utakaokuwa kitako cha Imani yao kwa kupitia uzoefu wa Mungu kupitia katika kisa chake.
- Wameanza kujenga mtazamo wa kilimwengu wa Biblia kwa kujifunza kisa cha Mungu
- Wameanza kupitia uzoefu wa uhusiano wa karibu na Yesu kila siku
- Wamefanya maamuzi ya kuchagua kuanza kumtumaini Yesu na kukubali msamaha wake.

**Angalizo kwa Waalimu:**

Pamoja kisa kwa kila somo, kuna fungu la kukariri kama sehemu ya tafakuri yetu kila siku. Mwisho wa kila somo, waombe wafanye maamuzi/kujitoa kikamilifu kufuata utendaji huu kila siku. Pitia na kuhimiza uwajibikaji kila wiki. Endelea kutumia hatua hizi kwa ajili ya kushiriki kisa kilichopo uk. Wa 9

### Sehemu ya 1: Jielekeze katika nguvu zisizo za kibinadamu.

**Somo la 1.** Kuna Mungu mmoja ambaye ndiye Muumbaji, aliye na nguvu, na mwenye rehema.

Kisa: Mungu ni Muumbaji (Mwanzo 1)

Kuna Mungu mmoja (Kutoka 20:2, 3, amri ya kwanza na ya pili)

Mungu ndiye mpaji na mkombozi wa watu wake (Torati 4:32-35)

Ombi la Hezekia (Isaya 37:14-16)

Pitia kisa kutoka katika masomo yaliyopita yanayoonesha kwamba majaliwa ya Mungu, ulinzi wake, rehema yake kwa Nuhu, Abraham, Yusufu, Ayubu, Daudi, na Danieli, n.k.

Usomaji wenye mwitikio: Zaburi 136:2, 4, 6, n.k. Kiongozi aseme (au kusoma) sehemu ya kwanza ya kila fungu, na hadhira kurudia, "Kwa upendo wake usioyumba, unaostahimili milele."

Fungu Elekezi: Zaburi 136:26

Kwa hiyo?

**Somo la 2: Yesu**: Yesu ni nani?

a. Kisa: Neno la Malaika kwa Mariamu (Luka 1:26-35)
b. Fungu Elekezi: Mathayo 16:16
   Kauli ya Petro kumhusu Yesu (Mathayo 16:13-17)
   Muhutasari (Waebrania 1:1-4; Wakolosai 1:15-20)
c. Kwa hiyo?

**Somo la 3: Roho Makatifu** – Anafanya nini?

a. Kisa: Wakati wa uumbaji (Mwanzo 1:1, 2)
   Ahadi ya Yesu ya kazi ya Roho Mtakatifu (Yohana 14:16-17, 25-27)
   Anabadilisha maisha (Wagalatia 5:22-25)
b. Fungu Elekezi: Matendo 1:8
c. Kwa hiyo?

**Somo la 4: Malaika** – Roho Njema

a. Visa: Hajiri (Mwanzo 21:14-21)
   Yakobo (Mwanzo 28:10-17)
   Viongozi wa Israeli (Kutoka 33:1, 2)
   Yusufu (Mathayo 1:18-25)
   Petro akiwa gerezani (Matendo 12:1-11)
   Kuzunguka katika kiti cha enzi cha Mungu (Ufunuo 5:11-13)
b. Fungu Elekezi: Zaburi 34:7
c. Kwa hiyo?

**Somo la 5: Maandiko Matakatifu** – Neno la Mungu lenye nguvu isiyo ya kibinadamu.

| | | |
|---|---|---|
| a. | Visa: | Mfano: Waumini katika Thesalonike (1 Thesalonike 2:11-13)<br>Timotheo (2 Timotheo 3:14-17)<br>Mafundisho ya Petro (2 Petro 1:16-21) |
| b. | Fungu la Elekezi: | Zaburi 119:105 |
| c. | Kwa hiyo? | |

**Somo la 6: Chanzo cha Uovu**

| | | |
|---|---|---|
| a. | Visa: | Lusifa (Shetani/Ibilisi) akiwa mbinguni (Ufunuo 12:7-9; Isaya 14:12-14; Ezekieli 28:12-17<br>Shetani kule Edeni, akimjaribu Adamu na Hawa: (Mwanzo 3:1-5, 14-15) |
| b. | Fungu Elekezi: | Mwanzo 3:15 |
| c. | Kwa hiyo? | |

**Somo la 7: Pambano Kuu mtazamo wa kidunia:** (Pambano kati ya Mungu na Shetani)

| | | |
|---|---|---|
| a. | Visa: | Ayubu (Ayubu 1:6-12; 2:1-7)<br>Vita mbinguni (Ufunuo 12:7-12) |
| b. | Fungu Elekezi: | Ufunuo 12:7, 8 |
| c. | Kwa hiyo? | |

## Sehemu ya 2: Uwezo wa Roho Waovu

**Somo la 8. Nguvu za Uovu/uwezo**

| | | |
|---|---|---|
| a. | Visa: | Yesu anawatuma wanafunzi wake na uwezo mkubwa (Luka 10:17-20)<br>Filipo akiwa Samaria (Matendo 8:4-8)<br>Vita ya kiroho (Waefeso 6:10-18) |
| b. | Fungu Elekiezi: | Waefeso 6:10:11 |
| c. | Kwa hiyo? | |

**Somo la 9: Matokeo ya kukosa kutii** – Hatia, aibu, hofu

| | | |
|---|---|---|
| a. | Kisa: | Adam na Hawa (Mwanzo 3)<br>Pitia visa vingine ambavyotumejifunza vinavyooensha matokeo ya dhambi. |
| b. | Fungu Elekezi: | Warumi 3:10-12 |

Kariri: Warumi 3:23

c. Kwa hiyo?

**Somo la 10: Njia ya Wokovu #1** – Kupitia katika kafara.

a. Visa: Adam na Hawa (Mwanzo 3:21)
Kaini na Habili (Mwanzo 4:1-5)
Abraham na Isaka (Mwanzo 22:1-14)
Israeli na Pasaka (Kutoka 12:1-13)

b. Fungu Elekezi: Waebrania 9:22

c. Kwa hiyo?

**Somo la 11: Njia ya Wokovu #2** – Kupitia kwa kafara ya Yesu

a. Kisa: Yesu kutundikwa msalabani (Marko 25:33-39)

b. Fungu Elekezi Yohana 1:29

c. Kwa hiyo?

**Somo la 12: Njia ya Wokovu #**3 – Nifanye nini nipate kuokoka?

a. Visa: Ujumbe wa Ezekieli (Ezekieli 36:25-28)
Ujumbe wa Paulo kwa Mfalme Agripa (Matendo 16:19, 20)
Ujumbe wa Paulo kwa waumini wa Rumi (Warumi 10:8-13)
Ujumbe wa Paulo kwa waumini wa Efeso (Waefeso 2:4-10)
Ujumbe wa Paulo kwa waumini wa Galatia (Wagalatia 4:4-7)

b. Fungu Elekezi: Yohana 3:16 au Waefeso 2:8, 9

c. Kwa hiyo?

**Somo la 13: Sabato #1** – Kusherehekea Uumbaji na Ukombozi katika Agano la Kale

a. Visa: Uumbaji (Mwanzo 1:27-2:3)
Mungu adondosha mana (Kutoka 16:1-8, 22-30)
Amri ya nne (Kutoka 20:8-11)
Ushauri kwa Israeli (Nehamia 13:15-19)

b. Fungu Elekezi: Torati 5:12-14 na Ezekieli 20:12

c. Kwa hiyo?

**Somo la 14: Sabato #2** – Kusherehekea pamoja na Yesu

a. Visa: Shughuli za Yesu siku ya Sabato (Marko 1:21-32; Luka 6:1-5)

Yesu na wanafunzi wake siku ya Sabato (Marko. 2:23-27; Luka 6:6-10)
Yesu aponya ndani ya Sinagogi siku ya Sabato (Marko 3:1-6; Luka 6:6-10)

b. Fungu Elekezi: Marko 2:27, 28
c. Kwa hiyo?

**Somo la 15: Hekalu** – Ni nini na umuhimu wake ulikuwa ni nini?

a. Visa: Kujenga hema ya kukutania (Pitia na kurudia Kutoka 25-27 ukitumia vielelezo
Kuhani alifanya upatanisho kwa dhambi (Walawi 16:32-34)
b. Fungu Elekezi Kutoka 25:8, 40
**c. Kwa hiyo?**

**Somo la 16: Hekalu mbinguni na Yesu Kuhani Mkuu**

a. Kisa: Yesu Kuhani Mkuu mbinguni (Waebrania 1:1-3; 4:14-16)
b. Fungu Elekezi: Waebrania 4:16
c. Kwa hiyo?

## Sehemu ya 3 – Kuelewa mambo ya Usoni

**Somo la 17: Kifo – Ni nini kinachotokea watu wanapokufa?**

a. Visa: Binti wa Yairo (Mathayo 9:8-19; 23-25)
Lazaro (Yohana 11:1-15)
Ujumbe wa Paulo wa tumaini kwa Waumini wa Thesalonike (1 Thesalonike 4:13-18)
b. Fungu Elekezi: 1 Thesalonike 4:16
c. Kwa hiyo?

**Somo la 18: Kuja mara ya pili kwa Yesu** na ishara za mwisho wa dunia.

a. Visa: Yesu akiongea na wanafunzi wake (Mathayo 24:3-14, 30, 31)
Ujumbe wa Yesu kabla ya kupaa kwake (Matendo 1:6-11)
b. Fungu Elekezi: Mathayo 25:31
c. Kwa hiyo?

**Somo la 19: Siku ya hukumu**

a. Visa: Mfano wa wanawali kumi (Mathayo 25:1-12)
   Mfano wa kondoo na mbuzi (Mathayo 25:31-46)
   Mfano wa talanta (Mathayo 25:14-30)
b. Fungu Elekezi: Ufunuo 14:7
c. Kwa hiyo?

**Somo la 20: Unabii – Kufahamu mambo ya usoni**

a. Visa: Ndoto ya Farao (Mwanzo 41:1-36 muhutasari)
   Ndoto ya Nebukadneza (Danieli 2:1-45, kwa muhutasari)
   Ahadi za Mungu (Yoeli 2:28,29
b. Fungu Elekezi: Amosi 3:7 na 2 Nyakati 20:20
c. Kwa hiyo?

Somo la 21: Mbingu na Nchi mpya

a. Visa: Njozi ya Isaya (Isaya 65:17-25)
   Njozi ya Yohana (Ufunuo 21:1-4; 22:1-5)
b. Fungu Elekezi
c. Kwa hiyo?

**Sehemu ya 4 – Kuwa sehemu ya kanisa**

**Somo la 22: Ubatizo** – Kujiunga na familia ya Mungu

a. Visa: Mfano wa Yesu na Yohana mbatizaji (Mathayo 3:13-17)
   Mkushi (Matendo 8:26-38)
b. Fungu Elekezi: Matendo 2:38
c. Kwa hiyo?

**Somo la 23: Huduma ya meza ya Bwana** – Kumbuka Yesu alichofanya kwa ajili yetu.

a. Kisa: Chakula cha jioni cha mwisho na wanafunzi wake (1 Wakorintho 11:23-26)
b. Fungu Elekezi: 1 Wakorintho 1:26
c. Kwa hiyo?

**Somo la 24: Kumrudishia Mungu Zaka na Sadaka**

a. Visa: Abraham (Mwanzo 14:14-20)
Ahadi ya Yakobo (Mwanzo 28:20-22)
Mjane mwenye nusu pesa (Marko 12:41-44)
Waumini wa Korintho (2 Wakorintho 8:1-15)
b. Fungu Elekezi: Malaki 3:10 na Zaburi 56:12, 13
c. Kwa hiyo?

**Sehemu ya 5 – Kuishi maisha ya Muumini**

**Somo la 25: Mtindo wa maisha wa Biblia** na ulaji wenye afya

a. Visa: Lishe ya asili (Mwanzo 1:29)
Chakula walichopewa waisraeli kwa sheria (Walawi 11)
Ushauri wa Paulo kwa waumini kuhusu kanuni za kuishi (Waefeso 5:15-21)
b. Fungu Elekezi: 1 Wakorintho 10:31
c. Kwa hiyo?

**Somo la 26: Ibada**/mikutano/kujumuika paoja

a. Visa: Ibada hekaluni (Kutoka 25:8)
Mfano wa Yesu (Luka 4:16-21)
Mfano wa Paulo kule Filipi (Matendo 16:11-13)
Mfano wa Paulo kule Thesalonike (Matendo 17:1-4)
b. Fungu Elekezi: Waebrania 10:24, 25
c. Kwa hiyo?

**Somo la 27: Kushiriki ujumbe wa matumaini**

a. Visa: Wito wa Ibrahimu kutoka kwa Mungu (Mwanzo 12:1-3)
Yona (Kitabu cha Yona kwa muhutasari)
Andrea (Yohana 1:35-42)
Wanafunzi wa Yesu (Matendo 1:1-8)
b. Fungu Elekezi: Mathayo 24:14 na Mathayo 28:19, 20
c. Kwa hiyo?

**Somo la 28: Nguvu na umuhimu wa maombi na tafakuri**

a. Visa: Daudi alifanya tafakuri (Zaburi 77:11-15)
Danieli aliomba mara tatu kila siku (Danieli 6:4-10)
Mfano wa Yesu – akiomba asubuni na mapema (Marko 1:35)
Yesu kule Gethsemane (Marko 14:32-38)
b. Fungu Elekezi: 1 Thesalonike 5:17 na Zaburi 1:1, 2
c. Kwa hiyo?

**Somo la 29: Kumtumaini Mungu wakati wa shida na dhiki** hata kama maombi yako hayakujibiwa.

a. Visa: Ayubu (Ayubu 1-2, kisa kwa muhutasari)
Yusufu (Mwanzo 37:12-36, 39-41 kisa kwa muhutasari)
Marafiki wa Danieli (Danieli 3)
Imani "Ukumbi wa umashuhuri" (Waebrania 11:32-39)
b. Fungu Elekezi: 2 Wakorintho 12:9; Ayubu 13:15; Danieli 3:17, 18
c. Kwa hiyo?

## Hitimisho la Suala hili

Katika masomo haya tumeangalia Imani za msingi ambazo ni muhimu sana ili kufanya wanafunzi na kuleta watu katika Imani itendayo kazi katika Yesu kama Waadventista wa Sabato. Hizi Imani hasa ni kwa wale ambao hawakuwa Wakristo hapo awali.

